

# TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA


Telegramu: COSTECH

Simu: +255 (022) 2771358

Mkurugenzi Mkuu: +255 (022) 2774023

Idara ya Utafiti : +255 (022) 2700749

Barua pepe: [dg@costech.or.tz](mailto:dg@costech.or.tz)



Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S. L. P. 4302

Dar es Salaam

Tanzania

## TAARIFA KWA UMMA

### MAELEZO KUHUSU MRADI WA MAHINDI YANAYOVUMILIA UKAME NA WADUDU WAHARIBIFU (WEMA/TELA)

Mradi wa WEMA (*Water Efficient Maize for Africa*) ulianza nchini mwaka 2008 kwa ushirika wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Idara ya Utafiti na Maendeleo (DRD) ya Wizara ya Kilimo, ambayo sasa imekuwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

### Sera, Sheria na Kanuni zinazongoza Utekelezaji

Nchi yetu ina *Sera ya Taifa ya Bioteknolojia ya mwaka 2010* yenye lengo la kuhakikisha Tanzania inanufaika na matumizi ya bioteknolojia kwa maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii. Pia tunayo *Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013* inayoainisha nia ya kutumia bioteknolojia kuinua uzalishaji.

Usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia yameainishwa chini ya *Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA Act, 2004)*. Sheria hii imetungiwa *Kanuni za Kusimamia Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa (2009)* na *marekebisho yake (2015)* na *mwongozo na mfumo wa usimamizi (2010)*. Utekelezaji wa mradi wa WEMA/TELA unazingatia malekezo yote yaliyoainishwa kwenye nyaraka hizo za kitaifa.

### Wadau, Malengo na Mafanikio ya Mradi

Mradi huu unashirikisha taasisi za Utafiti wa Kilimo za Nchi 6 za Afrika ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Msumbiji, Ethiopia na Afrika Kusini. Mradi wa WEMA/TELA unafadhiliwa na *Bill and Melinda Gates Foundation*, *Howard G. Buffett Foundation* na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) kupitia *African Agricultural Technology Foundation (AATF)*.

Lengo la mradi ni kuongeza usalama wa chakula kwa kuzalisha aina bora za mahindi yanayostahimili ukame na bungua wa mahindi katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mkakati wa utekelezaji wa mradi unajumuisha mbinu za kawaida za ugunduzi wa mbegu bora (*conventional breeding*) na bioteknolojia ya kisasa (*modern biotechnology*).

Baadhi ya mafanikio ya Mradi katika utafiti wa kutumia mbinu za kawaida yanajumuisha kugundua na kuidhinishwa aina 11 bora za mahindi chotara yanayostahimili ukame na kutoa mavuno mengi. Uzalishaji na usambazaji wa aina nne ambazo ni WE2109, WE2112, WE3113, WE3117 unafanywa na makampuni binafsi ya mbegu (Ultravetis, Agri Seeds na Jambe Seed). Aidha Wakala wa Mbegu wa Taifa (ASA) anategemea kuanza kuzalisha mbegu hizi kwa wingi na bei nafuu.

Mafanikio kwa utafiti wa kutumia teknolojia ya uhandisi jeni (GMO) ni pamoja na kuanzisha shamba maalumu (*Confined Field Trial site*) la kufanya utafiti wa mimea iliyoboreshwa kwa njia ya bioteknolojia ya kisasa kulingana na Kanuni za Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa (*National Biosafety Regulations*) katika Kituo cha Kilimo cha TARI-Makutupora.

### **Hatua zitakazofuata baada ya Kumalizika kwa Jaribio**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inaweka msukumo katika kufanya maamuzi ya kisera yenye kuzingatia ushahidi wa kisayansi. Hivyo, katika utekelezaji wa mradi huu wa WEMA/TELA, mbali na takwimu za mavuno, watafiti wanakusanya pia takwimu za usalama wa teknolojia kama vile (i) athari kwa mazingira (ii) usalama wa chakula kwa binadamu na mifugo.

Kadri sheria, taratibu na kanuni zinavyotuongoza, matokeo ya utafiti huu yatawasilishwa tena katika Ofisi ya Makamu wa Raisi – Mazingira kwa hatua zaidi. Ikiwa kutakuwa na suala la kisera, ni matumaini yetu kuwa wadau wote watahirikishwa kutoa maoni yao.

### **Mwito**

Ili kupata taarifa sahihi na za uhakika kuhusiana na utafiti huu, wadau wote wanakaribishwa kuwasiliana na COSTECH au TARI. Pia mnakaribishwa kutembelea shamba la majaribio kule Makutupora Dodoma ili kujifunza zaidi juu mradi.

**Imetolewa na:  
Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia  
06 Novemba, 2018**